Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Na unapowaona wale wanaozihafifisha Aya Zetu, basi ujitenge nao mpaka wazungumze maneno mengine; na kama Shetani akikusahaulisha, basi usikae baada ya kukumbuka pamoja na watu wadhalimu. (AL-AN'AAM 6:69)

JUZU 80 No. 218 | DH.QAD-DH.HIJ.1442AH | SEPTEMBA 2020 | IKHA 1399 HS | BEI TSH. 500/=

Muongozo wa Islam Uchaguzi Mkuu 2020

Na Amir & Mbashiri Mkuu

Hakika Allah Anawaamuruni kuzirudisha amana kwa wanaozistahili, na ya kwamba mnapohukumu baina ya watu mhukumu kwa uadilifu; bila shaka mawaidha Anayowatoleeni Allah ni mazuri sana; Hakika Allah ndiye Asikiaye, Aonaye.

Enyi mlioamini! Mtiini Allah na Mtiini Mtume Wake na wale wenye mamlaka juu yenu; na kama mkihitilafiana juu ya jambo lolote, basi lirudisheni kwa Allah na Mtume, ikiwa mnamwamini Allah na siku ya Mwisho. Hayo ni bora kwa matokeo. (4:59-60)

Sawa na Aya hizi Allah Ametuamuru waaminio kwamba katika mambo yahusuyo dini yetu tufuate maagizo yaliyotolewa Naye Allah katika Quran Tukufu na pia tufuate miongozo iliyotolewa na Mtume Wake s.a.w. katika sunna zake na hadithi zake sahihi.

Aidha katika mambo mengine yasiyo na mwelekeo wa moja kwa moja wa amri za kidini, na ambayo Allah kwa hekima zake ameamua kuyawacha mikononi mwa wanadamu, waaminio tumetakiwa pia kuwatii wale wenye mamlaka juu yetu.

Sawa na uelewa huu wa Aya hizi, na sawa na sunna na hadithi za Mtume s.a.w., katika mambo yahusuyo utawala, uongozi, sheria na kanuni za kuendesha nchi, waaminio tunaamrishwa pia kuzitii mamlaka zilizo juu yao hata kama viongozi wake sio Waislamu, maadam tu



sheria na kanuni hizo hazipingani na amri zilizo bayana za Allah na Mtume wake. Sehemu ya mwisho ya aya isemayo: na kama mkihitilafiana juu ya jambo lolote, basi lirudisheni kwa Allah na Mtume; inasisitiza jambo hili.

Kuhusu mtindo gani wa siasa ufuatwe na nchi fulani, inaonesha kwamba Allah Ameliwacha jambo hilo mikononi mwa wanadamu wenyewe, sawa na hali halisi ya maadamu tu utasimamishwa juu ya misingi ya haki na adili miongoni mwa raia. Ingawaje kwa kuzingatia agizo la Allah kwamba:

وَاَمۡرُهُمۡ شُوۡرٰى بَيۡنَهُمۡ ۪

Yaani waaminio ni wale ambao utendaji wao hufanyika kwa kushauriana wao kwa wao (42:39); basi inaonekana kwamba mtindo wa kidemokrasia unaotoa nafasi kwa wananchi wengi iwezekanavyo kuchagua viongozi wao, unapendelewa zaidi na Allah.

Hivyo kama inavyoeleweka na sisi sote kwamba, Inshallah ifikapo siku ya Jumatano tarehe 28 mwezi huu wa Oktoba, taifa letu tulipendalo kama mzazi wetu au zaidi, taifa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, litafanya uchaguzi wake mkuu; hatuna budi kulipokea jambo hili kwa moyo mkunjufu na shukurani.

Sawa na nidhamu ya Islam Ahmadiyya duniani kote, Jumuiya kama taasisi huwa haijiingizi katika siasa za nchi yoyote na kamwe haiwachagulii wala haiwashawishi waumini wake juu ya mwelekeo wowote wa kisiasa, bali kama raia wanayo haki ya kuelekea mrengo wowote waupendao na jumuiya huwa haiwaingilii juu ya hilo. Kikubwa ambacho Jumuiya daima huwataka waumini wake kukizingatia ni kwamba wawe watu wema na wenye mtazamo chanya kwa taifa lao na hivyo watumie vizuri akili na hekima zao kushiriki katika kuwaweka madarakani watu ambao kwa uelewa wao wanawaona wanaweza kubeba amana na dhamana ya uongozi, kwani juu ya jambo hili wataulizwa na Allah. Hii ni sawa na aya niliyoisoma mwanzoni:

Endelea uk. 2

Tanzania Yaendelea Kubarikiwa Anena Amir Jamaat

Na **Rajabu Abasi Mkieti**
Ikwiriri - Rufiji

Hayo yamesemwa na Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry Sahib katika hotuba yake ya kuhitimisha uhuisho wa Jalsa Salana ya Tanzania 2020 ambayo ilifanyika kuanzia tarehe 11 hadi 13 Septemba 2020. Mpango huo wa uhuisho wa Jalsa Salana ya Tanzania iliandaliwa na kuratibiwa na ofisi ya Amir Sahib, ilianza siku ya Ijumaa ambayo Amir Sahib alitoa hotuba ya ijumaa ambayo alieleza kua sawa na kalenda ya matukio siku hiyo ndio ilikua ni siku ya mwanzo ya Jalsa salana ya Tanzania 2020 lakini kutokana na sababu za janga hili la ugonjwa wa corona (COVID-19) kuziathiri shughuli za kijamii pamoja na ibada mwaka huu Jalsa Salana haitafanyika kwa hivyo



imeandaliwa mpango kama uliofanyika huko Uingereza wa kuhuisha Jalsa salana kwa njia ya mitandao ya kijamii. Hotuba hiyo ya Ijumaa ilirushwa mubashara pia zilirushwa hotuba mbalimbali katika ziku zote tatu ambazo zilizotolewa katika Jasla zilizopita ziku ya mwisho ya tatu ilitolewa hotuba ambayo ilirushwa mubashara kupitia mitandao ya kijamii. Katika hotuba ya Ijumaa Amir Sahib alieleza falsafa ya ndani juu ya kuanzishwa Jalsa salana ambayo alipitia maelezo mbalimbali ya Masih Aliyeahidiwa as Mwanzilishi

Endelea uk. 4

IMETOSHAA!!! uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

IMETOSHA

Ukiachilia mbali Afrika iliyotengenezwa na mkutano ule wa hovyo wa ukoloni wa 1884-85 mjini Berlin na hivyo kuweka mipaka ya uongo na kweli baina ya makabila mawili yanayozungumza lugha mmoja na utamaduni ule ule, Afrika iliyogawanywa na kupewa Wareno, Wajerumani, Wahispania na Wafaransa, Waingereza. Afrika ilivyowekwa chini ya serikari katili zilizotesa na kubagua na kuwanyonya wananchi. Afrika inayoendelea kuteseka chini ya mradi wa ukoloni mamboleo, jambo moja ambalo wameshindwa kutekeleza ni kwamba Afrika imebaki ni mwili mmoja. Na sehemu yoyote ya mwili ikiwa na maumivu mwili wote hauwezi kuwa sawasawa.

Maumivu yanayoendelea Nigeria na kuwafurahisha maadui wa Afrika ni maumivu yetu pia. Watu wanakufa na mali zinateketea. Kila Mnigeria mmoja akifariki Waafrika sote tumefariki. Nigeria inayo nafasi maalum katika bara la Afrika. Ni miongoni mwa nchi za mwanzoni katika kupata uhuru hivyo kutupatia matumaini kuwa inawezekana. Nigeria inafahamika kwetu pia kutokana na majina ya Dr Mnandi Azikiwe na Alhaj Sir Abubakar Tafawa Balewa kwani yaliwasha moto katika nyoyo zetu kupigania Uhuru wetu. Na Nigeria haikusinzia ilipopata Uhuru. Walipita huku na kule wakitetea nchi za Afrika ambazo zilikuwa hazijapata uhuru. Nigeria ilikuwa miongoni mwa nchi zilizoanzisha umoja wa Afrika mjini Addis Ababa mwaka 1963. Yalipotokea maasi ya jeshi nchini Tanzania Nigeria ilileta jeshi lake ili kusaidiana na ndugu zao Watanzania ili kujenga amani lakini Nigeria imewakilisha vizuri sana Afrika. Utajiri wake wa mafuta umeifanya nchi hiyo iwe na sauti katika mikutano ya kimataifa. Nigeria imerudisha heshima ya utamaduni wa Afrika uliopondwa na ukoloni mpaka wakoloni wakadiriki kusema kuwa Afrika haikuwa na utamaduni wetu. Aliyewaaibisha ni Chinua Achehe ambaye riwaya yake aliyoitoa 1958 *Things Fall Apart* ni ushahidi wa kutosha kwamba Afrika ina uwezo wa kutoa sauti yake yenyewe. Hatuhitaji mtu yeyote kutusemea. Wole Soyinka ni mwandishi wa kwanza wa Afrika ya weusi kujinyakulia zawadi maalum ya Fasihi ya Nobel Prize, Christopher Okigbo ni mshairi mahiri katika karne ya ishirini na hivi sasa tuna Chimamanga Ngozi Adiche ambaye riwaya zake *Half of the Yellow Sun* na *Americanus* ndio gumzo katika ulimwengu wa Fasihi duniani kwa hivi sasa. Dakika moja ya machafuko katika nchi hiyo inatuumiza sana.

Tatizo la Nigeria haliwezi kumalizwa na hao MaShylock ambao kila siku wanadai kipande cha mnofu wa binadamu. Ghasia kwa upande wao ni mtaji. Wanapata fursa ya kuuza silaha zao. Afrika inatakiwa ikae chini na kutatua tatizo hili ambalo si la Nigeria bali la Afrika. Majuzi Rwanda na Burundi walitupa matumaini tena kwamba tunaweza kutatua matatizo yetu sisi wenyewe. Mawaziri wa Nje wa nchi hizi mbili ambazo zimekuwa na uhasama walisema wahawahitaji mpatanishi kutoka nje. Watalimaliza tatizo ambalo si tatizo bali ni mabaki ya sumu yaliyoachwa na mkoloni. Sera ya mkoloni siku zote imekuwa 'wagawe uwatawale'.

Nani asiyejua kwamba kutokana na historia chafu ambayo Afrika imepitia haiwezi kupoteza hata nukta moja. Tumekwishapotezewa muda wetu mwingi. Wavamizi bila ya pasipoti waliingia katika bara hili na kuleta sintofahamu kubwa. Ukaingia utamaduni wa watu kupelekwa nje ili kutajirisha wengine. Ukaingia ukoloni. Tukanyonywa. Ukaja ukoloni mamboleo. Tukashangilia uzuri wa bendera zenye rangi na nyimbo tamu za mataifa yetu wakati huo wajanja wakihamisha utajiri wetu. Sasa tuna utandawazi ambao kwa jicho ambalo linatizama mambo kwa umakini, huo si utandawazi bali ni utandawizi. Tuamke na tuachane na biashara ya kuwafurahisha adui zetu.

Tunahitaji amani ili tujenge Afrika yetu. Allah Ibariki Afrika.

Muongozo kwa Wanajumuiya kuhusu Uchaguzi Mkuu

Kutoka uk. 1

إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَنْ تُؤَدُّوا الْأَمَانَاتِ إِلَىٰ أَهْلِهَا ۙ وَإِذَا حَكَمْتُمْ بَيْنَ النَّاسِ أَنْ تَحْكُمُوا بِالْعَدْلِ ۚ

Hakika Allah Anawaamuruni kuzirudisha amana kwa wanaozistahili, na ya kwamba mnapohukumu baina ya watu mhukumu kwa uadilifu; ...

Hivyo, sambamba na uchaguzi huu ninawaomba waumini wote wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini, pamoja na Waislamu wengine bali na wananchi wote watakaozipenda nasaha hizi wazingatie yafuatayo:

1. Kuhusu mahusiano ya mwaminio na nchi au Taifa lake, Mtume mtukufu s.a.w. ametufundisha kwamba:

حب الوطن من الايمان

... yaani *kuipenda nchi ni sehemu ya imani*.

Sawa na kauli hii ipendezayo, mtume s.a.w ametufundisha kwamba waaminio tusije tukadhani kuwa kuzipenda nchi zetu kunakwenda kinyume na imani yetu, bali kwa hakika hiyo ni sehemu ya imani na hivyo daima tunatakiwa tuzitumikie nchi zetu kwa upendo na heshima na daima tuzitendee kwa namna ambayo itaonesha kwamba kweli tunazipenda na kuzithamini. Daima tujitolee kwa ukweli na uaminifu kwa ajili ya maendeleo ya nchi zetu, hata ikibidi kutoa muhanga, mali zetu, heshima zetu na hata maisha yetu. Kushiriki katika mipango inayosaidia ustawi na mustakabali mwema wa nchi zetu kama vile kushiriki chaguzi mbalimbali ni sehemu ya kuonesha upendo wetu kwa nchi zetu. Katika hali ya kawaida, kususia mipango kama hii hakuoneshi chochote isipokuwa kisirani na moyo uliokunjamana, na kwa hakika mtazamo huo hauungwi mkono na mafundisho ya Islam.

Daima Allah anatuamuru kwamba:

وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَىٰ ۖ وَلَا تَعَاوَنُوا عَلَى الْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ ۚ

Yaani: *Na saidianeni katika wema na utawa, wala msisaidiane katika dhambi na uasi* (5:3).

Hivyo kila mmoja wetu aliye na haki ya kupiga kura namuomba ajitahidi kadri iwezekanavyo kufanya hivyo.

Kushiriki katika mipango ya nchi kisiasa ambayo itahakikisha tunawapata viongozi walio bora ni wajibu wa kila raia mwenye sifa ya kupiga kura ambayo katiba ya nchi yetu imempatia haki hiyo.

Hivyo nimshauri tena kila mmoja wetu aitumie haki yake hii vizuri na asiipoteze bure kwani baadae tukiwa hai, tutakuwa na kipindi cha miaka mitano kusubiria uchaguzi mwingine. Inshaallah.

2. Jambo la pili ninalowaombeni kulizingatia ni kuhakikisha kwamba mnafuata sheria, kanuni na miongozo yote inayotolewa na vyombo vinavyosimamia uchaguzi. Kama ambavyo imeelekezwa kwamba watu wapige kura na kisha waendelee na shughuli zao za maisha au wabaki majumbani mwao wakisuburia utangazwaji wa matokeo ya uchaguzi, basi ni muhimu bali ni lazima kufanya hivyo. Kupingana na wenye mamlaka katika mambo ambayo si kufuru, tena kwa namna ambayo inaweza kuvunja amani na usalama wa nchi si jambo lililofundishwa na Islam.

Katika hadithi moja maarufu imeandikwa kwamba:

٦٥٩ـ عَنْ أَبِي الْوَلِيْدِ عُبَادَةَ بْنِ الصَّامِتِ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ قَالَ: بَايَعْنَا رَسُوْلَ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَلَى السَّمْعِ وَالطَّاعَةِ فِي الْعُسْرِ وَالْيُسْرِ وَالْمَنْشَطِ وَالْمَكْرَهِ وَعَلَى أَثَرَةٍ عَلَيْنَا، وَعَلَى أَنْ لَا نُنَازِعَ الْأَمْرَ أَهْلَهُ إِلَّا أَنْ تَرَوْا كُفْرًا بَوَاحًا عِنْدَكُمْ مِنَ اللهِ تَعَالَى فِيْهِ بُرْهَانٌ وَعَلَى أَنْ نَقُوْلَ بِالْحَقِّ أَيْنَمَا كُنَّا لَا نَخَافُ فِي اللهِ لَوْمَةَ لَائِمٍ.

Imesimuliwa na Hadhrat Abul Walid Ubadah bin Swamit r.a. aliyesema: Tulifanya baiat ya Mjumbe wa Allah s.a.w. juu ya sharti kwamba tutasikia na tutatii katika dhiki na faraja, katika furaha na karaha, na hata kama wengine wanapendelewa kuliko sisi, na kwamba hatutagombana na wenye madaraka isipokuwa tukiona kufuru bayana ambayo juu yake tunayo hoja kutoka kwa Allah; na kwamba tutasema kweli tupu popote tulipo bila kuogopa lawama ya mwenye kulaumu kumhusu Allah (Bukhari).

Hivyo sawa na agizo la Mtume Mtukufu s.a.w. lililomo katika hadithi hii pamoja na hadithi nyingine ambayo aliwaagiza waaminio kumlilia Allah iwapo watawala hawawatimizii haki zao; ni juu ya kila mwaminio kutimiza wajibu wake (yaani kutoa haki ya viongozi kupata utii kutoka kwake) yeye mwenyewe binafsi, na iwapo anaona viongozi wanashindwa kutimiza wajibu wao (yaani kutoa haki kwa raia ambayo ni kuwafanyia kwa haki na uadilifu) basi asizidai hizo kwa namna inayoweza kuleta uharibifu katika nchi, bali azidai hizo kwa kumuomba Allah Mwenyewe, ambaye ndiye Hakimu wa mahakimu wote na Mfalme wa wafalme wote.

Hivyo ninamuomba kila mmoja wenu ahakikishe kwamba hashiriki kwa namna yoyote katika kitendo chochote kinachoweza kupelekea uvunjifu wa amani ya jamii au kinachoweza kumpatia madhara yeye mwenyewe na familia yake.

Aidha ninamuomba kila Mwahmadiyya, bali kila raia ambaye atakabidhiwa kusimamia jukumu lolote katika uchaguzi huu ajitahidi kulitekeleza hilo kwa moyo wake wote na kwa uaminifu wake wote, akielewa kwamba atawajibika mbele ya Allah kwa matokeo yoyote hasi ambayo yatatokana na utendaji wake mbaya na hatimae ataulizwa na Allah juu ya namna alivyotekeleza jukumu lake hilo.

3. Jambo la tatu ninaloomba tulizingatie sote ni lile nililolitaja kiasi fulani katika sehemu ya pili, yaani kumuelekea Allah kwa maombi ya kweli.

Endelea uk. 3

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Muongozo kwa Wanajumuiya kuhusu Uchaguzi

Kutoka uk. 2

Maombi ya kweli na yaliyojaa ikhlas ndio silaha kuu ambayo mwaminio anatakiwa kuishika daima. Katika mambo yetu yote makubwa na madogo hasa mambo yale ambayo yanao uhusiano mkubwa na mustakbali wa maisha yetu, Mtume s.a.w. ametufundisha kuomba dua ya Istikhara ambapo mwaminio huliweka jambo lake mbele ya Allah na kumuomba kwa unyenyekevu kwamba Amjaalie lililo na kheri zaidi.

Sisi wanadamu, kwa sababu ni dhaifu na hatuelewi mambo mengi, wakati mwingine tunaweza kulipenda jambo fulani lakini likawa na shari nasi na wakati mwingine tunaweza kulichukia jambo fulani lakini kumbe likawa ni lenye kheri kubwa nasi. Hii ni kama asemavyo Allah.

وَعَسٰٓى اَنۡ تَكۡرَهُوۡا شَيۡـًٔا وَّهُوَ خَيۡرٌ لَّكُمۡ‌ۚ وَعَسٰٓى اَنۡ تُحِبُّوۡا شَيۡـًٔا وَّهُوَ شَرٌّ لَّكُمۡ‌ؕ

.... na huenda mchukie kitu nacho ni heri kwenu, na huenda mpende kitu nacho ni shari kwenu. (2:217).

Hivyo ninamuomba kila mwaminio, bali kila raia, ajitahidi sana katika siku hizi na hasa katika siku za uchaguzi wenyewe kujitupa mbele ya Mola wake kwa unyenyekevu na kwa kwikwi na vilio katika sala zake za usiku na katika njia zingine za maombi, akiomba kwamba kupitia uchaguzi huu Allah Mungu Atujaalie matokeo yale yenye kheri zaidi kwa ajili ya Taifa letu na kwa ajili ya mustakbali mwema wa watu wake pamoja na amani na usalama wa nchi.

Kama ilivyo kanuni ya dua ya Istikhara, katika maombi haya, mtu anatakiwa aliweke jambo lake mbele ya Allah na kwa kumtegemea Yeye na bila ya upendeleo wowote au tamaa au ubinafsi, amuombe Allah kwamba Amwamulie jambo hilo na kisha ajiweke tayari kupokea na kuridhika na chochote ambacho Allah atampatia.

Kwa upande wa ofisi, tayari tumeshamwandikia Huzur Aqdas atba na kumuomba aikumbuke nchi yetu kwenye maombi yake katika kipindi hiki cha uchaguzi na Inshallah sisi sote tutabaki kwenye maombi kwa sura hii hii ya kumuomba Allah Atufanyie hisani Zake na Aturuzuku lile lenye kheri zaidi nasi kama Taifa.

Allah Atujaalie uchaguzi wenye kheri na baraka. Alijaalie taifa hili lipite vizuri kwenye kipindi hiki kigumu cha uchaguzi, na hatimae livuke kwa salama, amani, upendo na mshikamano. Amin.

Arusha washiriki Maonyesho ya vitabu Nanenane

Na **Sheikh Shafii Memon**

Arusha

Asalaam akaykum warahmatullah wabarakatuh

Alhamdulilah Sawa na taratibu za kila mwaka tumrshiriki katika hafla ya nanenane. mwalimu Suleiman mwalimu wa Arusha mjini alifuatilia eneo kule nanenane na kwa fadhili za Allah tulibahatika kupata eneo zuri.kwa hakika tuliona ni muujiza kwani si kawaida kwa siku Kama ile kuweza kupata eneo kwani washiriki walikuwa wameshagawiwa maeneo nasi eneo letu amabalo tulikuwa tunakaa miaka ya nyuma walishapewa watu wengine.basi waalimu tulifika usiku wa tarehe 3 huko Arusha na tukaenda moja kwa moja kwenye viwanja vya nanenane usiku uleule tulianza kujenga Banda letu.kwa fadhili za Allah tulifanikiwa kukamilisha ujenzi wa Banda saa 5usiku.siku ya pili tarehe 4 tulikamailisha kazi ya kupamba Banda let Kama vile kuweka mabango yenye maandishi ya Kalima juu ya Banda na mbele tuliweka kitambaa chenye maandishi ya "JUMUIYA YA WAISLAAM WAAHMADIYYA TANZANIA-KARIBU NANENANE ARUSHA". pia upande wa kulia tuliweka picha ya Masih aliyeahidiwa a.s na upande wa kushoto tuliweka picha ya Khalifa wa tano a.t.b.a.. picha hizi zilikuwa chanzo kizuri chaahubiri.kwani Kila aliyekuja kwenye Banda letu alitaka kujua kuwa picha zile ni za kina Nani na kupitia hapo tuliweza kutoa maelezo kuhusu ujaji wa Masih a.s na uwepo wa ukhalifa ktk Islaam.Tuliweka meza kubwa ya vitabu na tukapanga vitabu kwa utaratibu kwa kuzingatia maudhui na mada za vitabu.vitabu vya Masih a.s tulivipanga pamoja. na vitabu vingine pia tukavipanga ktk mpangilio ambao ulipendeza kwa watu waliotembelea bandani. watu wengi walivutiwa na ile Kalima tuliyoweka juu kwani ilikuwa na maneno ya kiarabu ya kalimat shahada na tafsiri yake kitu amabacho ilifanya Kila anayeiona atambue kuwa bada hili ni la waislaam.watu waliotembelea kwenye Banda letu baada ya kupata maelezo yetu pia tuliweza kuwakaribisha kuwa watakapofikiwa na wakati wa Sala Basi wasihangaike kutafuta mahali pa kusali kwa kutoka nje Bali waje bandani kwani tumetenga mahali maalum kwa ajili ya sala.basi watu wengi walikuwa wanakuja ktk vipindi vya Sala na kupata ibada Kisha kutushukuru Sana kwa hudumu nzuri ambayo hakuna WAISLAAM wengine wowote waliofanya hivyo...kuanzia siku ya kwanza tuliyoanza maonesho,yaani tarei4-8-2020 Banda letu lilipokea watu wengi waliokuja kuuliza maswali kuhusu Ahmadiyya na Islaam kwa ujumla.tuliandaa utaratibu mzuri wa kuwakaribisha watu waliopita,ambap mwalimu mmoja alisimama barabarani na vipeperushi Kisha anawakaribisha watu kwa upole na adabu Kisha mwalimu mwingine aliyopo bandani anawapokea na kuanza kuwapa maelezo kwa kuanza kuwaelezea kuhusu vitabu vilivyopo.Tulikuwa tunafanya hivi kwa kupokezana na Kila aliyekuja bandani kwetu tulihakikisha anapata maelezo na anatoka na vipeperushi vinne mikononi mwake na tunamsisitiza kuwa akavisome kwa umakini kwani vina ujumbe muhimu na mzuri. vipeperushi hivyo ni

"Atambulisho wa JUMUIYA YA WAISLAAM WAAHMADIYYA"

"Uislaam hauna uadui na Ukristo"

"Tusiwakashifu viongozi watakatifu wa dini zote"

"Jiepusheni na maana potofu za jihadi"

Wengi walikuwa wanavutiwa Sana na mada za vipeperushi hivyo na kuahidi kuwa watavisoma.

Siku ya tarehe 6-8-2020 alikuja mama mmoja wa kizungu kwenye Banda letu.tulimkaribisha kwa bashasha Kisha akaanza kupitisha macho kwenye vitabu. Baada ya dk takribani tatu tukiwa tumemuacha aendelee kuangalia vitabu alianza kuongea nasi kwa mshangao.. "Kumbe Kuna vitabu vizuri vya kiislaam ktka lungha ya kiswahili"!alishangaa Sana na aksema yeye ni mwalimu wa chuo Cha biblia huko Rombo Kilimanjaro-hajawahi kuona vitabu vingi vya kiislaam ktk lugha ya kiswahili.nasi tulimueleza pia ipo tafsiri ya Quran tukufu ktk lugha ya kiswahili Safi na tulimuonesha...ooh alishangaa Sana akasema kumbe inaruhusiwa kutafsiriwa kwa lugha zingine.. tulimfahamisha Quran ni maneno ya Mwenyezimungu ambayo ni muongozo kwa watu wa dunia nzima kwa hiyo ni lazima yaeleweke kwa watu wa lugha tofauti kwa hiyo ni lazima yatafsiriwe ktk lugha husika ili yaeleweke kwa watu.basi aliipenda Sana na akainunua. pia alipendezwa na kitabu Cha zawadi kwa wakrosto,aliuliza kwa Nini kimeandika zawadi,je kinagawiwa bure..tukamueleza kuwa Hilo ni jina lililopewa kitabu hicho kwa sababu mafundisho yaliyomo humo mengi yameelezwa kutoka ndani ya biblia,hivyo yamekuwa zawadi kwa ajili ya ndugu zetu wakristo. pia kitabu hicho alikinunua.kisha tulimpa vipeperushi.alivutiwa Sana na vipeperushi hasa vile vya.. Jiepusheni na maana potofu za jihadi na Uislaam hauna uadui na Ukristo.aliomba tumoe vipeperushi vingi iwezekanavyo kwani hii mada ya uadui ni muhimu mno na siku zakaribuni alikuwa na mjadala mkali na wanafunzi wake kuhusu mada.. wao wanafunzi wanadhani kuwa waislaam ni maadui zetu. sisi tulimpa vipeperushi 50 na akashukuru Sana na aliahidi kuwa ataenda kuvigawa kwa wanafunzi na Kama hvitatosha Basi atapiga photocopy ili Kila mmoja apate ujumbe huu mzuri. Nasi tumueleza kuwa ujumbe huu unatolewa na jumuiya Safi ya kiislaam iitwayo Ahmadiyya,jumuiya



Mbashiri wa Arusha, Sheikh Muhammad Shafi Memon akimpa mheshimiwa Anna Mgwira zawadi ya vitabu aliposhiriki maonyesho ya Nanenane jijini Arusha 2020.

Endelea uk. 4

Arusha washiriki Nanenane

Kutoka uk. 3

amabayo inahimiza maelewano na kuvumiliana ktk imani tofauti. basi alifurahi Sana na kuahidi kwa atajenga urafiki na uhusiano nasi na atatualika chuoni lwake tukatoe hotba kuhusu mada hiyo na akachukuaawasiliono yetu kwa furaha.pia kwa Fadhili za Allah tuliweza kufanya vipindi viwili vya redio live kutokea kwenye Banda letu.siku ya kwanza tarehe 6 tulifanya kipindi Cha dk 20 kwa kupitia Redio Arusha one fm ambayo inarusha masafa ktk Kanda ya kaskazini yote... ndani ya kipindi hicho tulieleza atambulisho wa Jumuiya ya waislaam waamhadiyya pamoja na kazi muhimu inayofanya hapa nchini na duniani kwa ujumla,pia,tulieleza sababu za kuwepo kwenye maonesho ya nanenane kuwa ni kufikisha ujumbe wa kwa watu wote

Pia tarhe 7 tulipata tena kipindi ktk Redio hiyo hiyo live kutoka kwenye Banda letu,na siku hiyo tulieleza mada ya Uislaam hauna uadui na ukristo ambapo ilipambiwa na kauli mbiu yetu ya Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote.mada hii iliwafurahisha na kuwashangaza hata watu wa Redio wenyewe kwani wanasema hawajawahi kuwasikia waislaam wakitoa maelezo ya upendo kwa wakristo Kama tuvlivyoeleza sisi.

Tarehe 8 kwenye Banda letu tutembelewa na mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro-mama Anna Mgwira. Nimempa zawadi ya vitabu vya Mgogoro wa dunia na njia kuelekea kwenye amani naYesu ktk India..alifurahia zawadi hiyo.

Tarehe09/08/2020 ilikwepo siku ya kilele ch sherehe za nanenane na mgeni rasmi alikwepo Mhr Abdallah Hamisi Ulega Naibu Waziri Mifugu na Uvuvi. Alhamdolilah kwrnye sherehe za kilele nimepewa nafasi ya kutoa utambulisho ya jumuiyya na nimempa mgeni rasmi zawadi ya Quran Tukufu na tafsiri lake. Alhamdolilah matukio imetokea kwamba nimepsta baadhi ya uhusiano na watu wa serekali.

siku ya tarehe 9 tupata kotambulisho Cha ushiriki kutoka ofisi ya Taso kwa kutambua ushiriki wetu Kama Taasisi ya kidini na kwa miaka mingi tumekuwa washiriki ktk category ya watoa elimu. Watu takriban 1100 walitembelea Banda letu na walipata ujumbe na vipeperushi 1220 tuligawa. Maonesho yalikuwa ya mafanikioakubwa na ilikuwa miongoni mwa njia za kufikisha ujumbe wa Masih na Islaam kwa ujumla.

Wasalaam

Jamia washiriki Nanenane

Kutoka uk. 12

yalifanyika mkoani Simiyu, na kwa upande wa kanda ya mashariki ambayo hujumuisha mikoa ya Dar es Salaam, Pwani,Tanga na Morogoro, maonyesho hayo yalifanyika mkoani Morogoro, Mkoa ambao ndipo kilipo chuo chetu cha Jamia Ahmadiyya Tanzania.

Kufanyika kwa maonyesho hayo mkoani hapa,imekuwa ni fursa adhwimu kwa wanachuo kutumia hiyo kufikisha ujumbe wa Masihi aliyeahidiwa a.s kwa njia ya kugawa vipeperushi,kuuza vitabu,kuzungumza na watu n.k.

Katika maonyesho ya mwaka huu,wanachuo wa Jamia Ahmadiyya waliboresha ushiriki wao kwa kuweka banda maalum katika viwanja vya Nane-nane vilivyopo nje kidogo ya Mji wa Morogoro kando kando ya barabara kuu iendayo Dar es Salaam.

Katika banda hilo vijana wetu walifanya kazi kwa kujitolea na kwa bidii kubwa sana tena kwa saa ishirirni na nne kuanzia tarehe 4 hadi 9 Agosti 2020. Pamoja na kuwepo banda hilo wengine walikuwa wakitembea viwanjani hapo na wengine mitaani.

Alhamdulillah, Allah Amepokea vyema bidii hizo, kwani kwa siku hizo za maonyesho zaidi ya vitabu 1,007 (zikiwemo Qurani Tukufu 5) vyenye thamani ya Tsh 1,124,000/= viliuzwa na zaidi ya watu thelathini na tano elfu walifikishiwa ujumbe wa Islamu na wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. Kwa kuzingatia jitihada na moyo wa kujitolea wa vijana wetu hawa na mafanikio yaliyopatikana, mheshimiwa mkuu wa chuo chetu cha Jamia Ahmadiyya Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatt sahib aliamua kuwatunukia zawadi maalum vijana wa makundi manne waliofanya vizuri zaidi katika uwanja huo.

Akiongea na wanafunzi, mkuu wa chuo alisema kuwa, anauthamini mchango wa kila mmoja wao katika mafanikio hayo, lakini ameamua kutoa zawadi kwa makundi hayo yaliyofanya vizuri zaidi ili kuwatia moyo waendelee na jitihada hizo pia kuwahamasisha wengine waweze kujitahidi siku zijazo.

Tanzania Yaendelea Kubarikiwa

Kutoka uk. 1

wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya aliyoyaeleza sababu ya kuanzishwa mpango huu wa Jalsa salana kuwa sio tamasha la kidunia bali ni mpango utakao wakusanya wachamungu ili kumkumbuka Allah ili kukuza vipawa vyao vya uchamungu na kuongeza elimu. Siku ya pili iwawadia hotuba za uhuisho wa Jalsa zilianza kurushwa muibashara hotuba ya kwanza ilikuwa ni *Kudhihiri kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s.* iliyotolewa na Sheikh Bakri Abedi Kaluta. Siku ya tatu ambayo ndio Ilikuwa ya mwisho ya uhuisho wa Jalsa hiyo Amir Sahib alitoa hotuba mubashara kutoka katika ofisi yake ambayo mwanzoni alianza kwa kunukuu aya zilizo ndani ya Qur'an Tukufu zinazo sema: Kwa hakika Allah Yu pamoja na wale wanaomcha, na wale wafanyao wema. (16:129).

... Na anayemwogopa Allah, (Allah) Humtengenezea njia ya kuokoka, Na Humpa riziki kwa mahali asipopatazamia; na anayemtegemea Allah, basi Humtoshea; .... (65:3-4). Mbele aliendelea kueleza kwa kina katika hotuba hiyo sababu ya kuwa chini ya Ukhalifa wake" .Hivyo aliendelea kusema kuwa ni lazima tutoe kipaumbele katika kukuza viwango vyetu vya uchamungu kwa kuwa waislamu wa matendo. Alinukuu maelezo ya Masihi Aliyeahidiwa as yanayotutaka kuwa waislamu wa matendo yanayosema: Jueni kuwa kukiri kwa ulimi tu si kitu mpaka kufuatane pamoja na vitendo kwa nia ya moyo wote... (Safina ya Nuhu).Mwishoni Amir Sahib alitoa takwimu ambazo Alllah ameendelea kuijalia na kuibarika Jamaat Ahmadiyya Tanzania kwa kipindi cha mwaka mzima katika idara mbalimbali tangia Jalsa ya mwaka jana ambazo ni:

1. Jumuiya imefika katika maeneo mapya 88
2. Jamaat mpya 10
3. Jumla ya Jamaat zote nchini 384
4. Misikiti mipya 8
5. Jumla ya Misikiti yote 219
6. Nyumba mpya za walimu na Wabashiri 5
7. Jumla ya nyumba zote za Wabashiri na walimu pamoja na zinazokodiwa. 126
8. Vipeperushi vilivyochapishwa na kugawiwa 197,918



kujiunga na jamaat Ahmadiyya ni zipi. Alisema nilazima tutoe shukurani zetu kwa Allah kujiunga jamaat kwanjia ya kuwa waisalmu wa matendo na sio wa maneno kwani sisi tumemkubali Masihi aliyoahidiwa as.Amir Sahib aliendelea kusema kuwa "Jambo la msingi na kubwa kabisa ambalo kila Mwanajumuiya anapaswa kulikumbuka na kulizingatia siku zote ni kuijali na kuienzi neema ya Allah tuliyojaaliwa kwa sura ya Masihi na Mahdi Aliyeahidiwa a.s. Katika zama hizi za mwisho, Allah Ametufanya sisi Waahmadiyya kuwa warithi katika ardhi kwa kutujaalia kumpokea na kumwamini Masihi na Mahdi Aliyeahidiwa a.s. na baadae

9. Watu waliofikiwa na ujumbe wa Ahmadiyya kupitia vipeperushi 249,156
10. Idadi ya maonyesho mbalimbali makubwa na madogo ya vitabu na maandishi ya Jamaat.1567
11. Watu waliofikiwa na ujumbe wa Ahmadiyya kupitia maonyesho haya 205,599
12. Baiat mpya 3,875
13. Idadi ya madarasa ya malezi na semina elekezi 4,961

Alikamilisha hotuba yake kwa kuiombea jamaat na dunia ili Allah Aikinge dunia dhidi ya majanga na changamoto mbalimbaliikiwamomaambukizi ya ugonjwa wa corona na Ajaalie mwakani shughuli zote za Jamaat zirejee kama awali. Amin.

Maisha ya Mtume Muhammad s.a.w



Inaendelea Kutoka toleo lililopita

Yalivyosimuliwa na Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad r.a. Khalifatul Masih wa pili

KAMARI NA UNYWAJI WA POMBE

Waarabu walikuwa wana tabia ya kunywa sana pombe na kwao kulewa hadi kupoteza fahamu, au kusema maneno ya kipuuzi haikuwa aibu bali ilikuwa ni sifa. Moja ya alama ya sifa za mtu mwenye kuheshimika ilikuwa pia ni kuwanywesha pombe kwa kiasi kikubwa marafiki zake na majirani zake. Ilikuwa ni lazima kwa matajiri kuandaa vikao vitano vya unywaji pombe kwa siku.

Kamari ilikuwa ni mchezo wao wa kitaifa. Lakini walikuwa wameifanya kuwa ni fani ya aina Fulani. Hawakuwa wakicheza kamari ili kuongeza mali zao, bali walikuwa wameifanya kamari kuwa njia ya kudhihirishia ukarimu na ukubwa. Kwa mfano wachezaji wa kamari walikuwa na mkataba huu kwamba yeyote atakayeshinda basi afanye tafrija ya kuwaalika marafiki na watu wengine kwa fedha alizoshindia. Wakati wa vita ni kamari ndio ilikuwa njia ya kukusanyia fedha.

Hata siku hizi, desturi ya kuchezesha bahati nasabu katika siku za vita inaendelea kukua. Lakini wale wanaochezesha tombola wa Ulaya na Amerika wanapaswa kufahamu kuwa sifa ya uvumbuzi huu inawaendea waarabu. Wakati kulipokuwa na vita, makabila ya Kiarabu yalikuwa yakichezeshana kamari, na Yule aliyekuwa akishinda, alikuwa akibeba sehemu kubwa ya gharama za vita. Kwa uchache, waarabu walijilipizia kukosa kwao starehe na nyenzo zingine za kidunia kwa kunywa pombe na kucheza kamari.

BIASHARA

Waarabu walikuwa ni wafanya biashara na misafara yao ya kibiashara ilikuwa ikienda mbali sana. Walikuwa wakifanya biashara huko Abbysinia (Ethiopia) na walikuwa pia wakifanya bishara huko Syria na Palestina. Wao walikuwa pia na uhusiano wa kibiashara na India. Matajiri wao walikuwa wakiyapenda sana majambia yaliyokuwa yakitengenezwa huko India. Nguo zilikuwa zikitokea zaidi huko Yemen na Syria. Biashara hizi zilikuwa mikononi mwa waarabu. Waarabu wengine, ukiacha wa kule Yemen na wale wa maeneo ya kaskazini, walikuwa wakiishi maisha ya kibedui (ya kuhamahama). Hawakuwa na miji yao wala vijiji vyao, bali makabila yao yalikuwa tu yameigawa nchi katika sehemu tofauti. Walikuwa wakihama hama ndani ya maeneo hayo. Sehemu Fulani ilipoishiwa na maji walihamia sehemu nyingine. Na walipiga kambi pale walipokuta maji. Kondoo, mbuzi na ngamia zilikuwa ndio raslimali zao.

Na walikuwa wakitengeneza nguo kutokana na manyoya yao, na walikuwa wakitengeneza mahema kutokana na ngozi zao na sehemu iliyokuwa ikibakia walikuwa wakiipeleka sokoni na kuiuza.

HALI, DESTURI NA SIFA ZINGINE ZA WAARABU

Wao hawakuwa wasiozifahamu fedha na dhahabu, bali fedha na dhahabu yalikuwa ni madini yaliyokuwa adimu sana kwao, kiasi ya kwamba watu wao wa kawaida na masikini walikuwa wakitengeneza mapambo yao ya vyombo vya udongo na vitu vya uturi. Walikuwa wakitengeneza mikufu kwa kutumia karafuu, mbegu za matikiti maji na matango pamwe na vitu vingine vya aina hiyo. Na wanawake wao walikuwa wakivaa mapambo haya na kutohitaji mapambo mengine. Ufuska na upujufu ulikuwa umekithiri. Wizi haukuwepo sana lakini ujambazi ulikithiri. Kuwapora wengine walifahamu kuwa hiyo ni haki ya taifa. Lakini pamoja na hayo, pengine hakukuwa na kaumu yoyote ile iliyokuwa ikizingatia kuitekeleza ahadi kuliko waarabu. Kama mtu yeyote alikuwa akija kwa mtu Fulani mwenye nguvu au kwa kaumu Fulani na kusema kwamba mimi naomba hifadhi yako, basi ilikuwa ni lazima kwa mtu huyo (aliyeombwa hifadhi) au kaumu ile (iliyoombwa hifadhi) kumpa hifadhi mtu huyo. Na kama kaumu hiyo isipompa hifadhi, basi ilikuwa imejidhalilisha mbele ya Waarabu wote.

Washairi walikuwa na mamlaka mno, kana kwamba walikuwa ni viongozi wa kitaifa. Ilikuwa ni muhimu sana kwa viongozi kuwa fasaha wa kuzungumza na ikiwezekana wawe pia washairi. Ukirimu wa wageni ulikuwa umefikia katika kiwango cha juu kabisa. Kama msafiri yeyote aliyepotea njia na kufika kwa kabila lolote na kusema kwamba mimi nimekuja kama mgeni wenu, basi wao, bila kusita, walikuwa wakimchinjia mbuzi, kondoo na ngamia. Wao hawakuwa wenye kutazama kuwa ni mgeni wa aina gani aliyewafikia, kwao, kufikiwa na mgeni ilikuwa ni namna ya kuongeza heshima ya kaumu yao. Na kaumu ilikuwa ikilazimika kumheshimu (mgeni) ili kujiongezea heshima. Wanawake hawakuwa na haki yoyote ile katika kaumu hiyo. Ndani ya baadhi ya makabila, ilikuwa ikifahamika kuwa ni jambo la heshima kwa baba kumuua binti yake. Wanahaistoria wamekosea kwa kuandika hivi kwamba bara Arabu nzima ilikuwa na desturi ya kuwaua mabinti zao. Desturi hii, kwa asili, haiwezi kuwepo katika nchi nzima, kwa sababu kama desturi hii ingeenea nchi nzima, basi vizazi vya nchi hiyo vingesalimikaje? Jambo la hakika ni hili kwamba, Uarabuni, India na nchi zingine zenye desturi hii, zilikuwa na taswira hii kwamba baadhi ya koo zilikuwa zikijiona kuwa ni zenye kutukuka au baadhi ya familia baada ya kujiona kuwa zimetingwa ndani ya matatizo ya kukosa wachumba wenye hadhi kwa ajili ya mabinti zao, basi walikuwa wakiwaua mabinti. Ubaya wa desturi hii umo ndani ya dhulma yake, sio katika jambo hili kwamba kaumu nzima ilikuwa ikiwaangamiza mabinti. Baadhi ya makabila ya Waarabu walikuwa na desturi hii ya kuwaua mabinti kwa kuwazika wakiwa hai na baadhi walikuwa wakiwaua kwa kuwakaba koo na baadhi walikuwa wakiwaangamiza kwa namna nyingine.

Mbali na mama mzazi, mama wa kambo hawakuwa wakithaminiwa na waarabu kama mama na hawakuwa wakiona ubaya wowote kuwaoa. Hivyo baada ya kufariki kwa baba, watoto wengi walikuwa wakiwaoa mama zao wa kambo. Desturi ya kuwa na wake wengi ilikuwa imeenea sana. Hakukuwa na kikomo chochote cha kuoa. Mtu pia aliweza kuwaoa madada wengi kwa wakati mmoja.

Walikuwa wakifanya dhulma kubwa kwenye mapigano. Wale waliokuwa wakiwachukia sana walikuwa wakiwapasua matumbo yao na hata kuyatafuna maini yao. Walikuwa wakiwakata pua na masikio yao. Walikuwa wakiyatoboa na kuyatoa macho yao.

Desturi ya utumwa ilienea sana. Walikuwa wakiwakamata watu wa makabila dhaifu walioishi kwenye vijiji vya jirani na kuwafanya watumwa. Watumwa hawakuwa na haki yoyote ile. Kila mwenye kumiliki watumwa alikuwa akiwatendea watumwa vyovyote apendavyo na hakukuwa yeyote wa kumuuliza. Hata kama akimuua hakukuwa na lawama yoyote kwake. Kama akimuua mtumwa wa mtu mwingine, hata hivyo alikuwa hawezi kupata adhabu ya kifo na alikuwa akijikomboa kwa kumpa fidia mmiliki wa mtumwa Yule.

Ilikuwa ni kanuni iliyokubalika kwamba ni haki kuwatumia vijakazi kama njia ya kutimizia matamanio yao ya kimwili. Hata vizazi vya vijakazi hao waliendelea kuwa watumwa. Na vijakazi waliopata vizazi waliendelea kubakia watumwa.

Kwa uchache kuhusiana na maendeleo na elimu, waarabu walikuwa nyuma mno. Waarabu walikuwa nyuma mno katika kuwahurumia na kuwatendea vyema watu wa mataifa mengine. Waarabu walikuwa nyuma mno ya watu wengine katika mahusiano mema kwa akina mama. Lakini bila shaka yoyote, baadhi ya sifa Fulani fulani binafsi na ushujaa vilipatikana ndani mwao, na vilipatikana kwa kiwango hiki kwamba huenda watu wengine wa zama hizo hawakuwa na mfano wake.

Bustani ya Washairi

KUA UYAONE.

1. Nina anza na Rabana, yu pekee duniani
Kwa jinale Subuhana, wanamuita manani
Ninawaasa vijana, siniulize kwanini
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

2. Wazazi lihangaika, wakavipata vya kwao
Wewe pia hangaika, na upate kama wao
Usiwe unaropoka, mali si zako za kwao
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

3. Usiwe unaropoka, ukatafute vya kwako
Hapo nyumbani ondoka, usije pata anguko
Kibaya zaidi Kaka, huwapendi ndugu zako
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

4. Huwapendi ndugu zako, unawapiga makonzi
Zile mali si za kwako, unawatia majonzi
Eti zako peke yako, kiherehere kama nzi
Kudeng'a denge'ni baho, kumwande kuna uvyele.

5. Mara Baba ana hiki, mara mama ana kile
Wageni hauwataki, singizia hiki kile
Moyo umetahamaki, kutwa kucha makelele
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

6. Kila saa baba yako, mara kanunua gari
Kiumbe una vituko, jiandae na hatari
Sijefika kokoriko, kapatwa na tahayari
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

7. Kalindima alinena, vile vitu ni vya kwake
Na akarudia tena, ndio msimamo wake
Natakiwa kupambana, mpaka kieleweke
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

8. Mwisho wa Moto Majivu, kuna siku utajuta
We endeleza uvivu, kisa tu umevikuta
Usijetoka mkavu, kusubiri kwenye tuta
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

9. Wasema wazazi wafe, upate kurithi Mali
Kwanini wewe usife, tena ukafie mbali
Umekaa kama tufe, pia mekosa akili
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

10. Hausaidii kazi, upo upo tu kiumbe
Hutaki kufanya kazi, mlaini kama embe
Huwaheshimu wazazi, unawapiga vijembe
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

11. Jishughulishe kijana, utumike kama Jembe
Nenda hata karakana, pale kwa Mzee Lumbembe
Tuletee danadana, uje uone kimbembe
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

12. Dhikrillah ndio dawa, kumkumbuka Manani.
Kazi sala kama kawa, usijifanye muhuni
Lazima tuende sawa, kwa miongozo kundini
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

13. Ukianza kufa wewe, wazazi watabakia
Wadogo zako wenyewe, watapata kutulia
Ulikuwa kama mwewe, kila kitu narukia
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

14. Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
Usijivike majoho, uache kimbelembele
Huna utulivu Roho, hufai kuwekwa mbele
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

15. Nashindwa kueleweshwa, na inakuwakuwaje?
Sala unapoamshwa, unasema kwani je?
Dawa ni kufurumushwa, utajua taishije
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

16. Kama kazi saidii, we unafaida gani?
Na unafanya bidii, ya kuishi hapo ndani
Wajitia uko hai, hubadiliki kwa nini?
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

17. Na vyombo hauvioshi, pindi vinapochafuka
Haupiki kisa Moshi, ubosi umetukuka
Na unajifanya Nyoshi, muziki usiku kucha
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

18. Ubosi umetukuka, unaishi kwa wazazi
Bado una ukibaka, kitambo huachi wizi
Ujibadilishe kaka, uza hata tangawizi
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

19. Baba ana Mali nyingi!, mjeuri mtaani
Vijembe navyo kwa wingi, wakejeli majirani
Eti utajiri mwingi, watamba barabarani
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

20. Wewe jiachie tuu, kuna siku utanyoka
Kiburi si Mali kitu, ni bora ukaongoka
Hamtabaki na kitu, Manani akivitaka
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

21. Koo linakukauka, kazi ya kujisifia
Jiangalie we Kaka, na muda unafifia
Mali zitaja ondoka, takuwa umefulia
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

22. Sisi sote ni ndugu, lazima kukumbushana
Hata ukane undugu, tumeungwa na Safina
Tabia hiyo bandugu, nami nasema hapana
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

23. Unajifanya wa moto, wala haushauriki
Wali moto mboga moto, mwendo mkiki mkiki
Ndugu taungua Moto!, kiburi kukimiliki
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

24. Hao wazee wakifa, shughuli imeshaisha
Waweza pata kifafa, Mali kizitaifisha
Nduguzo kina Hanifa, wataishi bila presha
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

25. Naweza pata kifafa, Mali kizitaifisha
Unavyopenda misifa, kwa watu kujionesha
Tayari wameshakufa, umebaki na bashasha
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

26. Umebaki na bashasha, maana litaka Mali
Wazazi wameegesha, wewe unawaza Mali
Kweli umeniangusha, ulivyokosa akili
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

27. Ngoja ukue uone, simaanishi ghorofa
Ujitume upambane, uje uzizibe nyufa
Fanya litekelemwene, uje upate maafa
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

28. Unajifanya mbabe, wenzako kuwakung'uta
Unatamba kwa utabe, Nguzo imara ukuta
Kama kweli ni mbabe, kapigane na Ukuta
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

29. Na una tabia mbaya, hata wazazi hawana
Na wala huoni haya, wazee kujibizana
Watu wanaimba kwaya, kikumbushwa unanuna
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

30. Ujana Maji ya Moto, kupoa hauchelewi
Usijione mtoto, kwa kufanya yasostawi
Takutana na msoto, pakuanza huelewi
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

Abdallah S. Kalindima (K-Mtoto)
kalindimasenior@gmail.com

KIFO.

HU! Japo kina umiza, Ndo hivyo hakikwepeki,
Chabaki kutushangaza, Wala hakitabiriki,
Mioyoni hudumaza, Kifo hakiombeleki,
Dah! Kifo cha huzunisha, Pia na kusikitisha.

Jamani inaumiza, Pindi kinaposikika,
Twa baki twa jiuliza, Kama kina epukika,
Kifo cha tujaliliza, Hofu na kuweweseka,
Mmmh! Kifo cha huzunisha, Kifo kifo tusamehe.

Nacho pia kiliumbwa, Kwa kutumaliza sisi,
Watu wote tutakumbwa, Kutengana zetu nafsi,
Ardhi nyingi zitachmbwa, Na tutaingizwa sisi,
Tena kweli kifo kipo, Hakuna kujidanganya.

Lo! Kifo hakibagui, Si mkubwa si mtoto,
Umbile hakichagui, Kipo hata kwenye joto,
Kinapokuja hujui, Kifo kama ka la moto,
Kifo hakina huruma, Yeyote cha Mchukua.

Cha sababishwa kwa mengi, Ajali magonjwa pia,
Tena cha ondoa wengi, Wabakiao walia,
Na cha sababisha mengi, Maumivu kutwachia,
Kifo si tumeumbiwa, Twa subiri chukuliwa

Abubakary Abdallah Mwita.
Mkurya halisi.

FUMBO FUMBUENI

Nasema pole mpendwa, Mola akupe shifaa
Hofu maumivu kutendwa,Vyazua kizaa zaa
Tuyaonayo mageni, Fumbo siriye ni nini

Dua kwa wano tutoka, Waacha pengo huzuni
Twaacha kwenye vichaka, Wachanga Mola twauni
Tuyaonayo mageni, Fumbo siriye ni nini

Wanatungo wenye tenzi, Medani tokolezeni
Kwa utashi na mapenzi, Fumbo hili fumbueni
Tuonayo ni mageni, Fumbo siriye Ni nini

SHUNDA MSHUNDIA WANA
DALUNI TANGA
shunda267@gmail.com

WEKA AKIBA SWAHIBA

Chochote takacho pata, usimalize kwa kula.
kidogo waweza kata, kukipeleka kwa mola.
na kingine tena kata, akiba weka mahala.
weka akiba swahiba, maisha yatabiriki.

Masihi O. Stambuli

KUNDI LA WATU SITA

1. Ewe Mungu wa huruma, nina toa shukrani,
Kwa kuweze kukisoma, kitabu kilo na shani
Cha Khalifa wadhama, kutoka kwake manani,
Ni kundi la watu sita, Ewe Mola libariki

2. Kitabu ukikisoma, kunazzidisha yakini,
Nayale yalokukwama, Khalifa kuyabaini,
Hivyo itazidi hekima, yadini yakee manani,
Ni kundi la watu sita, Ewe Mola libariki

3. Nakuomba kwa huruma, Wazidishie Imani,
Wapate afya na wema, Vitawale maishani,
Waache vizazi vyema, Vitumikie Dini
Ni kundi la watu sita, Ewe Mola libariki

4. Ukitaka kujua vema, Msaada has ani nini?
Ufikiri kwa hekima, humo mwako moyoni,
Msada ungeli kwama, ningekuwa na hali gani.
Ni kundi la watu sita, Ewe Mola libariki

5. Wazidishe hekima, Waitumikie Dini,
Gurudumu kusukuma, la Masihi wa manani,
Na Dini yako karim, Izidi kupata shani.
Ni kundi la watu sita, Ewe Mola libariki

6. Hapa sasaninakoma, nikubali ya manani,
Watu tupate kusoma, na ituzidi yakini,
Dua hii iwe njema, Vizazi iviauni,
Ni kundi la watu sita, Ewe Mola libariki

Hassan Sango
Jang-e-Muqaddas kwenye karatasi

RABI POKEA DUA

Rabi ipokee dua, ya Hassan bin Sango
Sita amewatmbua, kwa kazi ya udinpongo
Wajalie ya Jalia, Wazidishie ubongo
Wazidi kutafsiri, kazi bado zaidana

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)
Kiwalani, Migombani, Dar es salaam

Sungura na Kobe

Sungura alikuwa akimdhihaki kobe siku moja kwa kuwa na mwendo wa kigoi goi.

"Hivi huwa unafika mahala popote?" aliuliza kwa kicheko cha kebehi. "Ndio," alijibu kobe, "na nitathibitisha fikra yako hiyo potofu. Ninakwenda kushindana mbio na wewe na kukuthibitishia."

Sungura alifurahishwa sana na wazo la kushindana mbio na kobe, isipokuwa kwa raha ya kigezo cha makubaliano naye. Kwa hiyo mbwa mwitu, ambaye aliazimia kuwa mwamuzi, aliweka alama ya uwanja wa kushindania na kuwaamuru waanze mbio.

Mwanzoni sungura alitoweka kabisa machoni pa watazamaji, na kufanya kobe ajisikie vibaya licha ya kuwa lilikuwa jambo la hovyo kwake kushindana mbio na sungura. Sungura alijilaza pembeni ya mti kupata kausingizi kidogo hadi hapo kobe atakapojaribu kumfikia.

Kobe wakati huo huo akawa anajikongoja bila kukata tamaa taratiiibu tena bila papara, alipita ile sehemu aliyokuwa sungura amelala. Hata hivyo sungura aliendelea kulala kwa amani kabisa; na



alipokuja tu kuzinduka, kobe alikuwa tayari ameshafikia kwenye mstari wa ushindi. Sungura akakimbia kwa kasi zake zote; hata hivyo, hakuweza kumpita kobe kwa wakati muafaka.

Taratibu bila papara hushinda mbio.

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno 24 hapo chini kwa kuyazungushia na Penseli

Quran	Hija	Dhambi	Muslih
Saumu	Shawl	Wema	Mauud
Taraweh	Daku	Fasiki	
Ramadan	Futuru	Mwaminio	
Ikhlas	Sihr	Masihi	
Taw	Maombi	Alfazl	

F	F	U	T	U	R	U	N	B	L	D	B	Q	L	Q
T	T	W	E	M	A	M	N	Z	U	T	Z	X	P	D
T	V	A	Q	F	K	M	A	K	H	W	H	K	N	G
F	F	T	R	N	W	F	A	U	X	N	M	I	R	T
S	L	K	L	A	L	D	N	M	U	D	K	H	J	I
H	Y	B	N	A	W	P	Z	T	M	D	T	M	B	A
A	S	A	U	M	U	E	T	A	Q	W	A	M	T	B
W	M	I	F	M	K	L	H	V	B	Q	A	P	R	N
W	A	X	H	Y	R	F	H	S	H	H	V	T	A	L
A	O	M	Y	R	T	L	A	I	D	X	Q	R	M	Z
L	M	A	B	D	X	L	L	S	L	J	U	R	A	B
V	B	S	W	K	H	S	V	Q	I	Q	Y	W	D	D
C	I	I	N	K	U	B	H	X	R	K	J	Y	H	Q
Q	K	H	I	M	K	H	G	X	J	T	I	C	A	M
J	L	I	X	N	M	W	A	M	I	N	I	O	N	H

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Mkate wa Mchele

Na **Mtandao**



Mahitaji

Mchele vikombe 4 vya rice cooker

Tui vikombe 4 measuring cups

Sukari kikombe 1

Hiliki

Hamira

Namna ya Kufanya

Loweka mchele wako, mimi nimetumia basmat.

Ukishalowana usage pamoja na sukari, hamira, tui na hiliki mpaka uwe laini uwache uumuke.

Weka sifuria jikoni tia mafuta mimina mchanganyiko wako Kama dakika moja tu.

Halafu tia ndani ya oven mpaka uwive.

Utoe, uwache upoe kabisa ndio uutoe kwenye sifuria ikiwa sifuria si *nonstick*.

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA AS

Amri za Huruma

Hazrat Masih Mau' a.s anasema: Likumbukeni vyema jambo hili pia kwamba ziko Amri za Mwenyezi Mungu. 1. Ya kwanza ni hii kwamba usimshirikishe na yeyote, si katika dhati Yake, sifa Zake wala Ibada Zake. 2. Na ya pili, muwarehemu wanadamu wengine. Na mradi wa Hisani sio huu kwamba uwafanyie ndugu zako na Jamaa zako tu hisani, bali yeyote yule, Mwanadamu au Kiumbe yeyote miongoni mwa Viumbe wa Mwenyezi Mungu, bila kujali yu Baniani au Mkristo. Ninakuambieni kweli kuwa Mwenyezi Mungu Amechukua jukumu la kuwapatieni uadilifu; Hapendi mjifanyie wenyewe. Kadiri mtakavyokuwa na Upole, Huruma na Unyenyekevu, ndivyo Mwenyezi Mungu Atakavyofurahishwa nanyi. Wakabidhini maadui zenu kwa Mwenyezi Mungu. Kiama kipo karibu, hampaswi kufadhaishwa na matatizo hayo wanayokupeni maadui. Mimi naona kwamba bado mtapata usumbufu sana toka kwao, kwa sababu wale watu walio nje ya wigo wa ustaarabu ndimi zao hubwatuka kana kwamba bwawa limebomoka na kusababisha mafuriko, hivyo mfuata dini anapaswa kuudhibiti ulimi wake.

(Malfudhat, Jalada 9, uk. 164 - 165)

DARASA LA QUR'AN TUKUFU

NJIA YA MAFANIKIO NI YA TAABU NA SADAKA

Na **Musa Salum Mgeleka -** 0717 504 690

Je, mnadhani kwamba mtaingia Peponi na hali hamjafikiwa na mfano wa wale waliopita kabla yenu? YALIWASHIKA MASHAKA NA DHARA NA KUTETEMESHWA SANA hata Mtume na walioamini pamoja naye wakasema: Msaada wa Mwenyezi Mungu utafika lini? Sikilizeni! bila shaka msaada wa Mwenyezi Mungu uko karibu.
WANAKUUKIZA WATOE NINI. SEMA: MALI YOYOTE MTAKAYOTOA, basi ni kwa ajili ya wazazi na ndugu na mayatima na maskini na msafiri; na wema wo wote mnaoufanya, basi kwa yakini Mwenyezi Mungu Anaujua. Sura 2:215-216

KHAIR - MALI Masahaba wa Mtume s.a.w. waliposikia kuwa wao hawawezi kufanikiwa mpaka WAPITE KATIKA NJIA ZA TAABU NA SADAKA, kama vile watu wa zamani, mara wakauliza watoe nini. Mwenyezi Mungu akawajibu, mtatoa khair, yaani mali nzuri kwa wingi (Mufradat na Akrab).
Wakati fulani fursa ya Kujitolea Mali kwa njia ya SADAKA huwahaionekani au kupatikana maana humuoni wa kumpatia Sadaka. Na kwa kuwa Sadaka ni Daraja la Mafanikio ya Kimwili na Kiroho basi Allah Hutengeneza njia mbalimbali za kumfanya Mwanadaabu Afanikiwe. Mafanikio huhitajiwa baada ya shida kadhaa kiasi hiki kila mmoja hukata tamaa kabisa juu ya kufanikiwa kwake. Hapo ndipo Allah Anapokuambieni fursa iliyopo kuondokana na Shida zenu ni Kutoa SADAKA. Watu wanalalamika maisha magumu na shida za hapa na pale zisizotatulika na kila Jitihada za Kibinadamu zikigonga mwamba. Basi Jibu lake ni Kutoa Sadaka. Sababu mbalimbali za Kutoa Sadaka zimeelezwa hapa kwa WAZAZI na NDUGU (Hapa kuna Ndugu wa Damu, Ndoa - Nasaba, Dini na Jamaa na Rafiki zetu nao ni Ndugu) na YATIMA (Wasio na Uangalizi na Msaada mwingi zaidi wakiwategemea Binadamu wenzao) na WASAFIRI na MASIKINI (wenye Dhiki).

Leo hii kuna ndugu zetu, Watanzania wenzetu wamekumbwa na Maafa ya mafuriko ya Maji wakihitaji Msaada wa Hali na Mali kutoka kwetu. Fursa hii Adimu imepatikana kwetu ili tujitolee Sadaka na Tumuombe Allah juu ya Shida zetu waila Shida zetu Zitatugharikisha kama watu waliozingilwa na Jiwe ndani. Kilicho waokoa ni KHAIR walioitenda. Kila mmoja Alikuwa Akisimulia kwa Allah Khair alizofanya kuomba Msaada. Na sisi basi tutoe Sadaka na Kuomba Allah juu ya Matatizo yetu kwa Kueleza namna Sadaka yako inavyoenda Kuokoa Maisha ya ndugu zetu.
Hatujui kwa leo fursa nyingine ya Kutoa Sadaka itajitokeza lini kabla ya Shida zetu hazijatuangamiza. Wakati ni leo tuliyojaliwa fursa hii waila unaweza ukawa mtu wa kujuta wakati Shida ulipatiwa na Fursa ya Kuepukana nayo Ukapatiwa Funguo zake kisha Ukashindwa namna ya kuzitumia.
Sadaka zipo za namna nyingi na kila aina ya Sadaka hutumika kwenye Shida husika na sio kila Sadaka inahitajika kwa mazingira yote. Nabii Yunus a.s aliokolewa kutoka kwenye tumbo la samaki kwa sababu tu ya Kumtukuza Allah kwa wingi Surah 37:140-146 hivyo waliotingwa na Mafuriko ili wasigharikishwe wanapaswa kutoa Sadaka ya Kumtukuza zaidi Allah na Atawaondolea Shida zao, Inshaallah. Watu sisi ambao hatuna Mafuriko ila tuna shida mbalimbali basi tunapaswa Kutoa Sadaka ya Mali/ Fedha, Matibabu, Nguo, Watoto wako/ Wafanyakazi wako, Wake zako, Makazi, Chakula n.k na kisha Kila mmoja wake amlilie Allah na Shida zake kwa Sadaka yake.
Mtume s.a.w alisema Kila TAABU imeambatana na FARAJA na Kila baada ya Dhiki kuna Faraja na Wepesi. Sunan Tirmidhi, Ab waa bul swfatil Qiyaamati
Kanuni hii ya Furaha imeungana na Huzuni na kila baada ya Dhiki kuna faraja na wepesi ni Kanuni Dhihiri iliyo dhihirishiwa na Manabii na Watakatifu wengi. Kila kwenye Shida walishika SUBIRA na KUTOA SADAKA mfano wa Mafanikio ya Nabii Ibrahim a.s subira na sadaka ya Hajira na Ismaili.
Njia ya Kuyatatua Ikishindikana basi Shida huwa Maangamio. Mwanadamu amepewa Maarifa na Uwezo wa kukabiliana na shida mbalimbali utumeke ila kwa bahati mbaya ikiwa ni Adhabu ya Allah Haiondoki bila njia za Kimbingu yaani uwezo zaidi wa Kibinadamu unatakiwa kutoka kwa Allah. Na watu na Jamii iliposhindwa Kutambua Msaada wa Allah kwenye Matatizo basi matatizo yaliwaganda na kuwa Msiba na Maafa kisha waliangamia. Hivyo Shida zetu zisituangamize tutumie fursa ya Kujitolea SADAKA. Inshaallah

Mola wetu, tumiminie subira, na Utuimarishe miguu yetu, na Utusaidie juu ya watu makafiri. Amin

MATUKIO KATIKA PICHA



Mbashiri wa Mikoa Shinyanga na Simiyu akimpa zawadi ya vitabu vya Jumuiya Afisa wa Serikali mkoani Simiyu



Ugawaji vipeperushi na maonyesho ya vitabu katika Mkutano wa kumpokea Mhe. Makamu wa Raisi jijini Mbeya ulioandaliwa na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya wa Mbeya



Wanafunzi wa Jamia walioshinda katika maadhimisho ya siku ya michezo katika picha ya pamoja na Amir na Mbashiri Mkuu na watumishi.



Picha ya pamoja Amir na Mbashiri Mkuu pamoja na ndugu, jamaa na Amila katika hafla ya kumkaribisha Sheikh Hussein Ng'amilo Masjid Salaam



Mpango wa kujitolea damu salama ulioandaliwa na Majlis Khuddamul Ahmadiyya nje ya Masjid Salaam



Maonyesho ya Qur'an Tukufu yaliyoandaliwa na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Iringa



Sehemu ya wanajumuiya waliohudhuria Uhuisho wa Jalsa Salana ya Tanzania mwaka 2019 wakisikiliza hotuba ya ufunguzi iliyotolewa na Amir na Mbashiri Mkuu, Sheikh Tahir mahmood Chaudhry Masjid Salaam



Sheikh Mkuu wa Simiyu na Shinyanga alimtembelea Mheshimiwa Anthony John Mtaka Mkuu wa Mkoa Simiyu katika Ofisi yake. Alimtambulisha Jumuiya na alimpa zawadi ya vitabu vya Jumuiya

Thawabu na Faida za Waahmadiyya



Sheikh Muzaffar Durrani
Rabwah, Pakistan

Waahmadiyya wamepata heshima na thawabu nyingi kwa kumpokea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Seyidna Ahmad as aliyetumwa kama msadikishaji na msaidizi wa Mtume Muhammad saw. Seyidna Ahmad as akieleza heshima hizo ameandika katika kitabu chake kiitwacho Kuondoa wasiwasi.

Heshima tano:

Awali ni hii kuwa, wao wamejenga dhana njema kwa ndugu yao (Seyidna Ahmad as) na hawakumchukulia kuwa muongo, na hawakuruhusu kupenya moyoni aina yoyote ya shaka chafu dhidi yake. Kutokana na sababu hii wamestahiki kupata thawabu hii anayopata mtu katika hali ya kuweka dhana njema kwa ndugu yake.

Pili, ni hivi kuwa hao wakati wa kuikubali haki hawakuogopa kulaumiwa na yeyote mwenye fundo la lawama yake, wala hawakuzidiwa na jazba za nafsi. Ndiyo maana, kwa sababu hii wamestahiki thawabu, kuwa wao baada ya kuupokea wito wa haki na baada ya kusikia sauti ya mnadi mmoja wa kiungu wakaupokea ujumbe wala hawakusita kutokana na kikwazo chochote kile.

Ya tatu ni hii kuwa, kwa sababu ya kuamini msadikishaji wa bishara, wameondokana na wasiwasi wote unaozalika siku moja kutokana na kusubiri sana kwa muda mrefu. Na mwisho katika hali ya kukata tamaa husababisha kupotea imani. Na wale watu wema, sio tu kwamba wameepukana na hatari zilizoelezwa hapo juu bali ishara moja ya Allah na bishara ya Nabii wake kwa kuziona kutimia katika uhai wao wamezidi sana katika nguvu ya imani na kupata maarifa ya imani iliyokuwa imani ya kusikia tu awali. Sasa wameepukana na wasiwasi zote ambazo huwa zinazozalika mioyoni juu ya bishara hizo ambazo huwa hazifikii kutimia.

Yannenikuwahaokwakumwamini Mjumbe aliyetumwa na Mwenyezi Mungu wameepukana na zile kali na ghadhabu za Mungu ambazo huwa zinawapata waasi ambao huwa hawapati hisa yoyote isipokuwa kukadhibisha na kukataa.

Ya tano ni hii wamekuwa wamestahiki kupata zile neema na baraka zinazo wateremkia wale watu waaminifu ambao kwa mawazo njema wanamkubali yule anaekuja kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Hizi ndizo zile faida ambazo Inshallah kwa fadhili za Mwenyezi Mungu watazipata wale watu waliomkubali Imamu wa zama.

Dhana mbaya ya wapinzani:

Lakini wale watu wasiokubali wao wanakosa mema yote haya na fikra, hofu na wasiwasi wao huu ni batili kuwa katika hali ya kukubali dini itapata madhara. Siwezi kuelewa kwamba kwa sababu gani hasara inaweza kutokea kwa dini. Hasara ingekuwa katika sura hii kuwa kama angekuwa analazimisha kufuata elimu mpya ya Kiislamu kinyume cha mafundisho ya dini ya Islam; kwa mfano angeharamisha kitu kilicho halali au angehalalisha kilicho haramu. Au angebadilisha itikadi za kiimani zilizolazima kwa ajili ya ukovu, au angeongeza au kupunguza kitu katika vitendo vya kisheria kama vile sala, saumu, hija na kutoa zaka n.k. Kwa mfano mahali pa kusali sala tano angefanya mara kumi au angeacha ikawa mara mbili tu au saumu za mwezi mmoja angefaradhisha ziwe za miezi miwili au angepunguza, au angeelekeza ziwe pungufu zaidi ya hapo; Hapo bila shaka upungufu ungekuwepo bali ni kufuru na hasara. Lakini katika hali ambayo anasema hivi hivi mara kwa mara kuwa "enyi ndugu, mimi sikuja na dini mpya wala mafundisho mapya bali mimi natoka miongoni mwenu na ni Mwislamu kama ninyi. Na kwa ajili yetu sisi Waislamu, isipokuwa Kurani Tukufu hakuna kitabu chochote kile tunachoweza kukifuata au kuwaongoza wengine kukifuata. Wala hakuna kiongozi wala mfuatwa wetu mwingine ila yule Muhuri wa Manabii, Muhammad saw."

Hatuna wasiwasi:

Sasa kwa ajili ya Mwislamu mstawi yeyote kuamini dai lake hili lenye msingi wa ufunuo Kutoka kwa Allah, kuna pahali pa wasiwasi gani. Kwa mfano tu kama kashfi na funuo zake ni makosa na maagizo anayopewa yeye amedanganyika kuyaelewa, sasa kwa anayekubali kuna kosa gani? Je atakuwa amekubali jambo ambalo litamsababishia ufa wowote katika dini yake? Kama kweli kweli katika uhai wetu Hadhrat Isa Ibnu Mariam huyo huyo akishuka kutoka mbinguni, basi moyo wetu utafurahi na macho yetu yatangaara. Sisi kwa Jumuiya yetu itakuwa wa kwanza kumpokea na itapata thawabu ya kukubali jambo la awali lilolikubali kwa nia safi na kwa kumhofu Mwenyezi Mungu; hata hivyo katika hali ya kosa hilo pia (kama ikidhaniwa kuwa) hatua yetu ya thawabu itaendelea kuwa mbele. Sisi tumepata thawabu mbili na wapinzani wetu moja tu. Lakini kama sisi ni wakweli na wapinzani wetu ni wenye makosa kwa kuweka matumaini ya siku za baadaye basi imani za wapinzani wetu zimo katika hatari kubwa sana. Maana kama wao katika uhai kweli kweli wamemuona Nabii Isa bin Mariam katika hali ya jalali na utukufu anashuka kutoka mbinguni na wamemshuhudia kwa macho yao akishuka akiambatana na malaika, hapo ndipo imani yao itakuwa imesalimika, waila katika hali ingine ya pili imani haionekani itabakia salama. Kwani kama mpaka kufikia mwisho wa uhai wao mtu yeyote hakuonekana akishuka kutoka mbinguni bali wenyewe walikaribia kufa. Hivyo ni dhahiri kuwa watakwenda nazo shaka kemkem na juu ya bishara za Nabii Mkwelisaw wasiwasi za aina aina za wazi wazi zitazalika moyoni. Na ni karibu kuwa wasiwasi mkali wa aina fulani utokee utakaosababisha hata imani pia iangamie. Kwani zama hizi kwa mujibu wa ishara za Injili na Hadithi ni zama hizi hizi ambamo Masihi Mauud anatakiwa ashuke. Ndiyo maana miongoni mwa watawa waliopita wenye kashfi, ndani ya kashfi zao wamebainisha kuwa muda wa kuja kwa Masihi ni miaka ya mwanzoni mwa karne ya kumi na nne ya Kiislamu.

Mshusheni Masihi:

Hivyo basi kama Seyidna Ahmad as sio Masihi mauud, basi ninyi watu mshusheni Masih Mauud kutoka mbinguni. Basi ninyi mu wazao wa watawa, kaeni msikitini muombe dua kwa unyenyekevu mkubwa kuwa Isa Ibnu Mariamu aje kutoka mbinguni huku ameweka mikono juu ya mabega ya malaika ndipo mtakuwa wakweli waila kwa nini basi ninyi mnafanya dhana mbaya pasipo na haki na mnakuwa mnakuja chini ya tuhuma ya aya hii: Usifuate usiyo na elimu nayo. (Banii Israaiil, 17:37) Muogopeni Mwenyezi Mungu.

Kwa fadhili ya Allah Jumuiya yetu ni Jumuiya jema ambalo kwa wakati wake limemkubali mamuri aliyetumwa na Mungu wa mbingu na ardhi. Na mioyo yao haikuona ajizi yoyote katika kukubali kwa sababu wao walikuwa wema na Mwenyezi Mungu amewachagua kwa ajili yake, Mungu Akawapa nguvu na wengine hawakupewa na akawafunulia vifua vyao na wengine hawakufunulia. Hivyo basi wale waliochukua, hawa wataongezewa zaidi, lakini wale ambao hawakuchukua vitachukuliwa kwao walivyokuwa navyo hapo kabla. Waongofu wengi walitamani kuwa wazione zama hizi, lakini hawakuweza kuziona. Lakini ni masikitiko kuwa watu hawa wameona lakini hawakukubali.

Mfano wa wapinzani:

Kuhusu wao mfano huu unatosha kuwa hivi kwamba mfalme mmoja kwa mujibu wa ahadi yake akamtuma mtawala mmoja kwenye mji fulani ili aone kwa hakika mtii ni nani? Na asietii ni nani? Na ili magomvi yote yaliyomo ndani yao yaamuliwe. Hivyo basi mtawala huyu akafika katika muda huo huo uliokuwa lazima kwake, naye akawafikishia ujumbe wa kiongozi wake na akawaita wote kwa njia iliyoongoka na akadhihirisha kuwepo kwake hakimu. Lakini hao wakapata mashaka juu ya kuwa kwake mtumishi wa serikali, ndipo akawaonyesha alama zinazohusiana na watumishi wa serikali tu. Lakini wao hawakuamini wala kumkumkubali nao wakamtazama kwa mtazamo wa karaha nao wakajiona wakubwa na wakakataa kumkubali kama hakimu. Bali wakamshika na kumfedhehesha na wakamtemea mate usoni, na wakakimbilia kumuua. Wakamwona mnyonge na duni na wakamwona hakiri na wakampinga kwa matusi makali. Kisha baada ya kuteswa sana kwa mikono yao iliyopangwa naye akarejea kwa mfalme wake. na wale watu wote waliomfanyia vibaya kiasi hicho wakaendelea kumsubiri mtawala mwingine aje na njia ya ujahili wakaendelea kudumu kwenye mawazo haya haya batili kuwa huyu hakuwa mtawala bali yule ni mtu mwingine atakaekuja ambaye sisi tunatakiwa kumsubiri. Hivyo basi wakamsubiri mtu huyo mchana kutwa nao walikuwa wanasimama na kumchungulia kuwa atakuja lini na waliendelea kuizungumzia ahadi ya mfalme, na waliendelea kumsubiri tu mpaka jua likaanza kuzama na hakuna yeyote aliekuja. Hatimaye karibu ya jioni maaskari polisi wengi wakafika walikuwa wamebeba pingu pia na walipofika tu wakachoma mji wa wasumbufu. Wakiwashika wote, kila mmoja akatiwa pingu nao wakashtakiwa kwa kwenda kinyume na amri halali ya dola na kujaribu kupambana na vyombo vya dola, na hapo wao wakapata adhabu waliostahili.

Hivyo nasema kweli kweli kuwa hivyo ndivyo itakavyo kuwa hali ya wakataaji wakosefu wa zama hizi. Kila mtu atashikwa kutokana na makosa ya ulimi wake, kalamu yake na mikono yake. Mwenye masikio na asikie.

Siku za Michezo Yawa Kivutio Jamia Ahmadiyya

Kwa fadhili za Allah,wanachuo wa chuo chetu cha Jamia Ahmadiyya waliadhimisha siku za michezo kwa siku mbili mfululizo,katika siku za Jumatano na Alhamisi tarehe 23-24/09/2020. Mgeni rasmi katika shughuli hizo alikuwa Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry.

Maadhimisho hayo yalifanyika katika viwanja vya chuo vilivyopo Kihonda katika Manispaa ya Mji wa Morogoro, kwa kufanyika fainali za michezo mbalimbali kama vile:- Kuruka umbali mrefu (long jump), kuruka juu (high jump), kuruka kichurachura riadha mita mia moja na mita elfu moja na mia sita,mbio za miguu mitatu,mpira wa wavu,mpira wa meza,mbio za viunzi,kukimbia na gololi katika kijiko,kukalia kiti,nguvu za miguu na mikono na mpira wa miguu.

Michezo hiyo yote ilifanyika kwa kiwango cha juu na ilikuwa kivutio kikubwa kwa watazamaji hata wa nje pia. Mabingwa wa jumla ni timu ya Shuja'at chini ya uongozi wa Sheikh Ahmad Daud sahib na msaidizi wake Mwl. Kassim A. Mgalu sahib, wakati ambapo waliokuwa mabingwa watetezi timu ya Amanat wao walitwaa ubingwa wa mpira wa miguu na kuambulia nafasi ya pili, huku timu ya Shafqat ikiambulia nafasi ya tatu na kutwaa ubingwa wa shindano jipya la Barri.

Maadhimisho hayo yalihitimishwa siku ya Alhamisi tarehe 24/09/2020 kwa hafla fupi iliyofanyika chuoni hapo. Hafla hiyo ilianza kwa usomaji wa Qur'an Tukufu



Timu za Shafqat, Amanat na Shuja'at wakipewa risala kabla ya kuanza mashindano

iliyosomwa na Ustadh Salim Omar sahib na kufuatwa na shairi la Kiswahili ambalo lililosomwa na bwana Yaqini Rajab Sandali. Baada ya shairi ilifuata usomaji wa ripoti fupi ya hafla hiyo katika lugha ya Kiswahili na kisha ripoti hiyo katika lugha ya ki Urdu ambayo ilisomwa na Sheikh Azeez Ahmad Shahzad sahid.

Baada ya ripoti hiyo,mgeni rasmi Amir na Mbashiri Mkuu Nchini aligawa zawadi kwa washindi mbalimbali na kutoa nasaha chache kwa wanafunzi na wahudhuriaji wote kwa ujumla.

Katika nasaha zake, Amir sahib alisoma aya ya mia moja arobaini na nne kutoka katika Suratul Baqara isemayo, "*Na kila mtu anayo shabaha anayoielekea, basi shindaneni katika mema…*"

Kisha Amir sahib anasema kuwa anakumbuka tangu Jamia imehamia Kihonda kutoka katikati ya mji wa Morogoro imekuwa ikipata maendeleo makubwa na haraka kila mwaka na haya yote yamechangangiwa na ushirikiano uliopo baina ya Mkuu wa chuo na watumishi wote na hivyo kuwataka waendelee na ushirikiano huo.

Kuhusu wanafunzi, Amir sahib amesema kuwa pamoja na michezo na mashindano mbalimbali,lakini kamwe wasisahau shabaha ya wao kuwepo hapa chuoni. Alisema kuwa wao ni vijana kutoka katika nchi mbalimbali hivyo waishi kwa ushirikiano bila ya kubaguana na wadumishe nidhamu na khulka njema na kutia bidii katika masomo ili wawe watumishi wazuri wa Jama'at na Islam.

Mwisho mgeni rasmi aliongoza maombi ya kimya na kufunga hafla hiyo. Kisha wahudhuriaji walisali sala ya Maghrib na Ishaa,na baada ya sala chakula cha pamoja kiliandaliwa kwa wanachuo na wageni wote.

Watu Walio Bora Kabisa: Masahaba wa Badr

Kutoka uk.12

yule akajibu wewe umeshaniambia habari hizi mara kadhaa huko nyuma. Ndipo Mtume saw akiwageukia upande wa hadhrat Abu Musa na Bilal ra akawambia mtu huyu ameikataa bishara aliyopewa basi ninyi wawili ipokeeni. Wao wakajibu sawa sisi tumeikubali. Ndipo Mtume saw alipoagiza kuletwa bakuli lenye maji. Naye akanawa mikono, kisha uso kisha akasukutua na akawaambia kunyweni humo, na miminiyeni maji yake usoni na kifuani kwenu. Ndipo walipofanya sawa na walivyo amriwa na Mtume saw. Hadhrat Umme Salama ra alikuwa nyuma ya pazia akawaambia bakisheni kiasi cha maji kwa ajili ya mama yenu yaani yeye (mke wa Mtume saw) Ummul mo'miniin. Kwa hiyo wakabakisha kiasi kidogo kwa ajili yake.

Inasimuliwa kutoka kwa hadhrat Ali ra kwamba Mtume saw alisema kila nabii hupewa wasaidizi saba (naqiib) nami nimepewa wasaidizi 14. Miongoni mwao ni hadhrat Bilal pia.

Kuna hadithi nyingine ambamo Mtume saw alisema Bilal ni mtu wa aina gani! Yeye ni kiongozi wa waadhini wote na watakaomfuata nyuma yake ni watoao adhana, na siku ya kiyama watakaokuwa na shingo ndefu ni wanaotoa adhana.

Kuna hadithi nyingine ambamo Mtume saw alisema Bilal ni mtu wa aina gani! Kwani yeye ni kiongozi miongoni mwa mashahidi na wanaotoa adhana na siku ya kiama mtu atakayekuwa na shingo ndefu ni hadhrat Bilal ra, yaani yeye atapata cheo cha juu chenye heshima kubwa.

Katika simulizi nyingine Mtume saw amesema siku ya kiyama hadhrat Bilal atapewa ngamia jike mmoja atakayetokana na ngamia majike wa peponi, naye atapanda juu yake.

Mke wa hadhrat Bilal anasema kuwa Mtume saw aliwahi kusema jambo lolote mtakaloambiwa na hadhrat Bilal litakalokuwa limetoka kwangu basi jambo hilo ni la kweli, naye hatakuambia jambo la uwongo. Kwa hiyo wewe usimkasirikie hata mara moja. Kwani kadiri utakavyo muudhi hadhrat Bilal ndivyo itakavyo kataliwa kukubaliwa vitendo vyako.

Inasimuliwa kutoka kwa hadhrat Abu Huraira ra kuwa Mtume saw alisema mfano wa hadhrat Bilal ni ule wa nyuki anayetua na kunyonya kwenye matunda matamu na machachu. Lakini asali inayotengenezwa kutokana nayo ni tamu tupu.

Kuna simulizi moja ya hadhrat Bilal ambamo Mtume saw ametoa nasaha kwa hadhrat Bilal kwamba ewe Bilal penda ufe maskini lakini usipende kufa tajiri. Akamuuliza Mtume saw hali hii itatokeaje? Mtume saw akamjibu riziki yoyote unayojaaliwa usiitunze mwenyewe bali uigawe kwa watu na chochote unachoombwa usikatae. Hadhrat Bilal akauliza kama mimi sikuweza kufanya hivyo kutatokea nini? Mtume saw akamjibu ni lazima iwe hivyo kama nilivyo sema vinginyevyo makazi yako yatakuwa motoni. Khalifa mtukufu atba anaielezea hadithi hii kwa kusema yeyote anayeomba usimfukuze na mali unayoipata usiihifadhi bali itowe kwa kuwagawia watu wengine.

Kifo cha hadhrat Bilal kilitokea wakati wa ukhalifa wa hadhrat Umar ra katika mji wa Damascus nchini Syria. Alipofariki alikuwa na umri wa miaka zaidi ya 60.

Hadhrat Muslih Maud ra anasema safari moja watu walikusanyika katika mji wa Damascus na kwa bahati katika siku zile hadhrat Umar ra pia alikuwa amekuja kule. Watu wakamwomba amwambie hadhrat Bilal atoe adhana. Ndipo alipomwambia Bilal kutoa adhana. Hadhrat Bilal akajibu wewe ni Amiri na khalifa wa waaminio. Kama wewe utaniamuru nitatoa lakini moyo hautaweza kuvumilia. Ndipo aliposimama na kutoa adhana ileile aliyokuwa anatoa katika wakati wa Mtume saw. Wakati yeye anatoa adhana watu walikuwa wanakumbuka zama za Mtume saw kwa hiyo walianza kulia na hadhrat Bilal pia yeye mwenyewe alikuwa analia. Hadhrat Bilal alipomaliza tu kutoa adhana akazirai palepale na baada ya muda mchache akafariki.

Khalifa mtukufu atba anasema huu ni ushahidi hai wa ukweli wa hali halisi iliyopo kama vile Mtume saw alivyosema hakuna tofauti kati ya Mwarabu na Mwajemi (asiyekuwa mwarabu) na ushahidi huu ni wa watu wasiokuwa Waarabu ambao waliitikia na kupokea sauti ya Mtume saw iliyokuwa na upendo mkubwa. Na ujumbe ule walioupata uliwapa yakini na kuamini kuwa taifa lao halikuweza kuwapa mapenzi sawa na mapenzi yale waliyoyapata kutoka kwa Mtume saw.

Khalifa mtukufu atba anasema huyu ndiye bwana wetu hadhrat Bilal ambaye alionesha mfano wa uaminifu na mapenzi ya kweli kwa bwana wake Mtume saw, na aliyetumia nguvu zote kukalisha na kustawisha mapenzi ya umoja wa Allah moyoni mwake na akaonesha mfano wake kwa vitendo vyake, mambo haya yote ni mfano mwema na mtakatifu wa kuiga kwa ajili yetu. Na masimulizi ya matukio mengi ya upendo wa Mtume saw kwa mtumishi wake hadhrat Bilal haupatikani sasa na wala hautopatikana hapo baadae mfano wake sehemu nyingine yoyote duniani. Ni jambo hili pekee linaloweza kuimarisha upendo katika dunia yetu ya leo. Na utaleta udugu na mshikamano na kuvunjilia mbali minyororo ya utumwa. Kwa hiyo wokuvu na ukombozi wetu upo katika jambo hili tu kwamba tufuate mifano hii ya mapenzi ya kweli kwa umoja wa Allah na Mtume wake saw. Allah Atujaalie uwezo wa kufanya hivyo. Amin.

Baadae khalifa mtukufu atba aliongoza sala ya jeneza ya marehemu mbalimbali waliofariki. Miongoni mwao ni bwana maulana Talib Yaqoob sahib wa Trinidad, Engineer Iftekhar Ali Qureshi sahib aliyekuwa Wakilul Maal wa Tatu wa zamani wa Pakistan, Bi Radhia Sultana sahiba wa Pakistan na bwana Muhammad Tahir sahib wa Qadian na kijana wetu Akil Ahmad mtoto wa Mirza Khalil Ahmad mwalimu wa Intenational Jamia ya Ghana.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

MUHAR.-SAFF. 1442 AH | SEPTEMBA 2020 | IKHA 1399 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufusaw

Imesimuliwa na Hadhrat Anas r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Alama mojawapo ya Saa ni kwamba watu watajifaharisha katika misikiti. (**Abu Dawud**).

Watu Walio Bora Kabisa: Masahaba wa Badr

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 25/09/2020 iliyotolewa Masjid Mubarak, Islamabad, UK; baada ya Tashahhud, Ta'awwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu, Hadhrat Amir ul Mu'miniin, Mirza Masroor Ahmad*atba* (**'A**yyadahullahu **T**a'ala **B**i-Nasrihil **A**ziiz') alisema;

Habari za hadhrat Bilal zilikuwa zinaendelea. Mtume saw alisikia kishindo cha kutembea kwa mtu mbele yake katika ndoto na akatambua mtu huyo alikuwa hadhrat Bilal. Baada ya kuamka Mtume saw alimwuliza hadhrat Bilal ni tendo gani ulilolifanya katika Islam lililokufanya wewe kutembea mbele yangu peponi. Kwani mimi nimesikia kishindo cha nyayo zako ukitembea peponi mbele yangu. Hadhrat Bilal akamjibu mimi sikumbuki ni kitendo gani haswa ila tendo moja mimi nakumbuka hudumu kulifanya. Mimi mara zote ninapomaliza kutawadha sikosi kusali nafali sawa na hiyari na uwezo wangu.

Kuna simulizi nyingine kwenye hadithi moja kuwa Mtume saw katika njozi aliona pepo imeletwa mbele yake akasikia kishindo cha nyayo za mtu anayetembea mbele yake. Mtume saw akamwuliza malaika Jibril mtu huyo ni nani? Akamjibu huyo ni hadhrat Bilal. Habari ya kisa hiki ikafika kwa hadhrat Abu Bakar siddiq ra. Yeye akasema laiti kama mimi ningekuwa mahala pa Bilal yaani baba yake Bilal angekuwa baba yangu na mama yake angekuwa mama yangu na mimi ningekuwa Bilal.



*Masjid Mubarak: Hadhrat Khalifatul Masih V*atba* huhutubia Ijumaa kwa waaminio tokea na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.*

Khalifa mtukufu atba anasema angalieni daraja la ubora wa hadhrat Bilal, yaani yule Bilal aliyekuwa anaburuzwa na watu mitaani kwa sababu ya unyonge na udhaifu wake, kwamba hadhrat Abu Bakar siddiq ra anatamani mahala pa hadhrat Bilal angekuwa yeye.

Hadhrat Muslih Maud ra akitoa hutuba kwa akinamama anasema ile kazi mtakayoifanya ninyi kwa ajili tu ya Allah itabaki milele. Leo sisi hatujui wazao wa hadhrat Bilal wako wapi, na wala hatujui kuwa wazao hawa wenyewe wapo au hawapo, na kama wapo wako sehemu gani, yaani miji yao iko wapi na raslimali zao ziko wapi?

Lakini adhana ile aliyoitoa katika msikiti mtakatifu wa Mtume saw mpaka leo imebaki hai nayo itaendelea kuwa hai dumu daima na huu ndiyo wema unaoendelea kudumu milele.

Khalifa mtukufu atba anasema hadithi zilizosimuliwa na hadhrat Bilal ni arobaini 40. Kati ya hizo nne zinapatikana katika kitabu cha Bukhari na Muslim. Kuna simulizi moja kuwa Mtume saw aliwahi kusema kuwa mimi nina shauku na kutamani kukutana na watu watatu peponi nao ni hadhrat Ali ra, hadhrat Ammar ra na hadhrat Bilal ra.

Safari moja hadhrat Umar ra alikuwa anaeleza ubora wa hadhrat Abu Bakar ra naye akafanya ishara kwa hadhrat Bilal. Naye akasema huyu ni hadhrat Bilal ambaye ni kiongozi wetu. Naye ni moja ya tendo jema la hadhrat Abu Bakar kwa sababu hadhrat Abu Bakar siddiq ra alimweka hadhrat Bilal huru kutoka katika utumwa.

Katika hadithi moja Mtume saw alimwambia hadhrat Abu Bakar ra kuhusu hadhrat Salman, Suhaib na hadhrat Bilal ra kwamba ukiwachukiza hawa umemchukiza Allah.

Kuna simulizi moja kuwa bedui mmoja alikuja kwa Mtume saw akamwuliza je ile ahadi uliyoifunga kwangu hutaitimiza. Mtume saw akamjibu pokea habari njema. Bedui

Endelea uk 11

Tunda jingine lawasili kutoka Ghana



Na **Rajabu Abasi Mkieti**
Ikwiriri - Rufiji

Kama wasemavyo waswahili kuwa mti hujulikana kwa matunda yake. Basi kijana mwingine ambalo ni tunda lililozaliwa kutoka katika Jamia tul mubashireen Ghana amewasili akiwa tayari amehitimu mafunzo ya elimu ya juu ya shahada ubashiri Sheikh Hussein Yusuf Ng'amilo.Sheikh Ngamilo sahib anakuwa ni mbashiri wa tatu kutoka katika chuo hicho cha Ghana kabla yake wabashiri watatu ambao niwa zao la chuo hicho ni Sheikh Shabani Shunda na Sheikh Musa mashiri.Sheikh Ngamilo alijiunga Jamia Tanzania 10 Oktoba 2010. Mwaka 2014 akachaguliwa kwenda nchini Ghana katika chuo hicho alicho hitimu mwezi wa tisa na saa kumi kamili alasiri aliwasili katika chuo hucho nchini Ghana. Alianza masomo na kuhitimu mwezi wa 6 mwaka 2020 walio maliza katika chuo hicho nchini Ghana wanafunzi 8 wa 4 toka Indonesia mmoja Burkina Faso, mmoja Kenya, mwingine Uganda na Tanzania lakini kutokana na sababu ya ugomjwa wa Corona(COVID-19) Sheikh Ngamilo akachelewa kurudi nchini mpaka tarehe 12 mwezi wa 9 mwaka huu 2020 ndipo alipo pata fursa ya kurudi Alhamdulillah.

Jamia Ahmadiyya Tanzania washiriki katika maonyesho ya Nanenane



Na **Sheikh Abid Mahmood**
Jamia

Kwa Zaidi ya miaka Mia moja thelathini na moja iliyopita Hazrat Masihil mau'ud a.s alipata Wahyi usemao kuwa "Mimi nitafikisha ujumbe wako mpaka pembe zote za dunia"

Tangu wakati huo hadi sasa,wanajumuiya wa waislamu wa Waahmadiyya wamekuwa wakitumia fursa mbalimbali zinazopatikana katika maeneo yao kwa minajili ya kufikisha ujumbe wa Hazrat Masihil-Mau'ud a.s.

Jitihada maalumu zimekuwa zikifanyika kwa shabaha hii na Allah ametia Baraka nyingi katika harakati hizi zote-ambapo matokeo chanya na matunda mazuri hupatikana mfululizo.

Moja kati ya mikusanyiko mikubwa katika nchi yetu ni ikiwemo maonyesho ya wakulima al-maarufu, "Nane nane".Kitaifa maonyesho hayo mwaka huu

Endelea uk 4